KUINGIZWA KWA ZAO LA KAHAWA NA KUANZA KWA KILIMO CHAKE KATIKA JAMII YA WAMERU WA KASKAZINI MWA TANZANIA

Na Dr Catherine BAROIN

Makala hii imeandikwa na Catherine BAROIN, mwezi Oktoba 1994, Meudon-Ufaransa na kutafsiriwa mwezi Agosti 2014 na Mwalimu P. B Basimaki, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha-Tanzania.

UTANGULIZI

Kuingizwa na kuanza kwa kilimo cha kahawa katika jamii ya wa-Rwa au Wameru wanaoishi upande wa Kusini Mashariki mwa miteremko ya Mlima Meru, Kaskazini mwa Tanzania[1], ambao ni jamii ya wakulima wenye idadi ipatayo 250,000, kunaonyesha waziwazi historia na maendeleo ya kilimo cha biashara barani Afrika. Kimsingi, kufanikiwa kwa kilimo hicho cha kahawa miongoni mwa Wameru ni matokeo ya sera za Ukoloni ambao ulikuwa umeimarika katika jamii hiyo ambapo Wakoloni walitaka kilimo hicho kiwanufaishe wao zaidi. Hali hiyo siyo ya kipekee japo ni tofauti na sehemu kubwa ya hali ilivyokuwa katika maeneo mengine ya Afrika ambapo kilimo cha biashara kilikuwa kikiendeshwa na wazawa baada ya kulazimishwa na wakoloni na siyo wakoloni wenyewe waliokiendesha.

Kuanzia mwaka 1954 na kuendelea, Wameru walikuwa ndio waanzilishi wa mfumo mpya wa kimaendeleo ambapo kupitia kiongozi wao wa kijadi walimleta mtaalamu kutoka Marekani na kumlipa kwa ajili ya kuwasaidia Wameru juu ya kuendeleza kilimo chao cha kahawa. Kufika kwa mtaalamu huyo kulileta mafanikio makubwa, jambo ambalo ni la kujivunia sana ikilinganishwa na ilivyozoeleka kuwa miradi mingi ya maendeleo barani Afrika haifanikiwi.

[1] Wameru wa Tanzania ambao kwa lugha yao wanajiita wa-Rwa, hawana uhusiano wowote na Wameru waishio Mlima Kenya.

1. Kilimo cha biashara katika jamii za Afrika

Unapozungumzia kuhusu kilimo cha biashara katika makoloni ya Kifaransa ya Afrika Magharibi unazungumzia juu ya kilimo cha kulazimishwa, jambo ambalo ni tofauti katika jamii ya Wameru ambao wanaishi Mashariki mwa Afrika: Ni Wameru wenyewe ndiyo waliojiingiza katika kilimo cha biashara cha zao la kahawa licha ya kuwekewa vikwazo na Wakoloni waliokuwa wakiishi katika eneo hilo pamoja na utawala wa kikoloni wenyewe ambao walitaka kukifanya kilimo cha kahawa kuwa ni kwa ajii ya manufaa yao pekee.

Ni ukweli usiopingika kuwa njia za Ukoloni zilizotumika katika maeneo hayo mawili ya Afrika zilikuwa tofauti. Kilimo cha biashara katika nchi za Afrika zinazozungumza lugha ya Kifaransa kilianzishwa kwa njia za kulazimisha kama ambavyo inajulikana vyema kwa wengi (Coquery-Vidrovitch, C. & Moniot, H. 1984; Suret-Canale, J. 1964, Vol. 2). Waafrika walilazimika kuingia katika kilimo cha biashara kutokana na kuwepo kwa amri ya Wakoloni iliyowataka kulipa kodi kwa kutumia fedha taslimu. Hivyo, wananchi walilazimika kujishughulisha na kilimo cha biashara ili kupata pesa za kulipa kodi. Pindi njia hiyo ilipoonekana kuwa haileti ufanisi, njia nyingine za moja kwa moja zaidi zilitumika: uanzishwaji wa viwango vya lazima vya uzalishaji wa zao la biashara ambapo pale mkulima aliposhindwa kufikia kiwango hicho aliadhibiwa.

Baadaye mazao hayo ya biashara yalikuwa ya manufaa makubwa hasa baada ya wafanyabiashara na makampuni kuanza kuyanunua kutoka kwa wakulima. Hata hivyo, kutokana na wafanyabiashara na makampuni hayo kuhodhi soko, wafanyabiashara hao walipanga bei za chini sana kiasi kwamba

kilimo cha biashara kikawa hakina faida ya kina. Hatua hiyo pia ilisababisha wakulima kukata tama na kuishia tu kulima kiasi kidogo cha mazao ya biashara kwa ajili ya kumudu kulipa kodi, jambo ambalo ni moja ya sababu ya kudumaa kwa kilimo hicho cha biashara katika maeneo mengi.

Tofauti na ilivyokuwa katika nchi za Afrika Magharibi, ukoloni katika nchi za Afrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza ulihusisha zaidi Wakoloni wenyewe kuja kuishi kwa wingi na kulima wao wenyewe ili kujipatia faida kubwa kwa kulima mashamba makubwa ya mazao ya biashara. Sehemu kubwa ya ardhi ilichukuliwa kwa ajili ya mashamba ya Wakoloni wa Kizungu na Waafrika walilazimika kufanya kazi katika mashamba hayo kama vobarua. Ili kujipatia faida kutokana na kilimo hicho, Wakoloni hao walihakikisha wanatumia mbinu za kisasa za kilimo na kudhibiti uzalishaji na uuzaji wa mazao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na bei nzuri ya mauzo ya mazao hayo. Katika mfumo huo wa uzalishaji, Waafrika walitengwa: vibarua wa mashambani walilipwa mshahara kidogo na wengine hawakuruhusiwa hata kuingia katika mashamba hayo ili kujipatia ajira.

Hata hivyo uendeshaji wa mashamba makubwa ya wakoloni ulitofautiana kulingana na maeneo: kwa kawaida walichukua ardhi katika maeneo yenye rutuba na yanayokidhi miradi yao ya kilimo. Kutokana na kigezo hicho, kiwango cha wakulima wa kikoloni kilikuwa kikubwa zaidi nchini Kenya kuliko Tanganyika na pia kiwango kilikuwa kikubwa nchini Tanganyika kuliko Uganda (Buijtenhuijs, R., 1971:51). Pale wakulima hao wa kigeni walipokuwa wengi, walidhubutu hata kuwazuia wakulima wa Kiafrika waliotaka nao kulima mazao ya

biashara kama wao ili wapate kupunguza ushindani. Hii ndiyo sababu hadi kufikia miaka ya 1950, Wakoloni waliwazuia wazawa wa Kiafrika wa Rhodesia ya Kusini (sasa Zimbabwe) na Kenya kulima mazao ya biashara yanayosafirishwa nje ya nchi ambayo ni tumbaku kwa Rhodesia ya Kusini na kahawa, chai na pareto kwa Kenya (Mosley, P., 1983: 40). Kwa mujibu wa mwandishi huyo ni kwamba nchini Kenya, 'Waafrika walizuiwa kulima kahawa kwanza kwa kutozwa ada, na pale kikwazo hicho kilipoonekana hakitoshi, utawala wa Kikoloni uliamua kupiga rasmi marufuku ya kilimo hicho, hadi pale marufuku na ada hiyo vilivyoondolewa mnamo mwaka 1949' (Mosley, P., 1983:40).

Hivyo katika maeneo hayo yaliyokuwa na uwekezaji mkubwa wa Wazungu katika kilimo, siyo kutokana na kulazimishwa kwa wazawa kushiriki katika kilimo cha mazao ya biashara kisicho na faida kama ilivyokuwa kwa nchi za Afrika Magharibi, bali ni kutokana na Waafrika kuvutiwa na faida kubwa ya kilimo hicho kilichokuwa kikifanywa na Wazungu na hivyo kufanya juhudi za makusudi kupambana na vikwazo vya Wazungu ili nao waweze kulima mazao hayo ya biashara. Miongoni mwa changamoto kubwa zilizokuwa zikiwakabili wakulima wa Kiafrika zilikuwa siyo tu uwezo wa kuzalisha mazao ya biashara bali pia namna ya kupata masoko ya bidhaa zao kama ilivyokuwa kwa Wazungu. Kwa ujumla, historia ya kilimo cha kahawa nchini Tanzania na Kenya inajijenga katika msingi huo hapo juu.

Hata hivyo, mchanganuo wa maendeleo ya kilimo cha biashara una mapungufu kadhaa. Kwanza, hakuna ukinzani wa moja kwa moja na uliokamilika katika historia ya kilimo cha

biashara barani Afrika baina ya nchi zinazongumza lugha ya Kifaransa na zile zinazozungumza Kiingereza. Katika kitabu hicho hicho, utafiti wa Jean-Pierre Chaveau kuhusu historia ya kilimo cha kakao nchini Ghana, Kodivaa (Ivory Coast) na Nigeria kuanzia mwishoni mwa karne ya 19, ni mfano mzuri wa kuanzishwa kwa kilimo cha biashara bila ya kulazimishwa, mfano ambao unaonyesha kufanana kwa michakato hiyo ya kuanzishwa kwa kilimo cha baishara katika sehemu hizo mbili ambazo zilitawaliwa na Wakoloni wawili tofauti. Hata hivyo, kuwepo kwa idadi kubwa ya Wakoloni katika nchi nyingine zinazozungumza lugha ya Kifaransa kuliwafanya Wakoloni hao kujaribu kuhodhi kilimo cha biashara kama ilivyokuwa katika kilimo cha kahawa katika pwani ya kati-mashariki nchini Madagaska (Fremigacci, J., 1982) na katika jimbo la Kivu nchini Congo ya Kibeligiji ambayo sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo- DRC (Hatungimana, A., 1993).

Kinyume chake ni kwamba, katika maeneo ambayo Wakoloni walikuwa wachache, waliwahimiza wazawa kuendesha kilimo cha biashara. Kwa mfano, kustawi kwa haraka kwa kilimo cha kahawa aina ya robusta katika jamii ya Wahaya wanaoishi kaskazini-mashariki mwa Tanzania kulitokana na mtindo huo wa kuhimizwa kufanya kilimo cha mazao ya biashara (Ilife, J., 1979:281-). Kwa hali hiyo ni wazi kuwa ushawishi wa kisiasa wa Wakoloni ndiyo kigezo kikubwa katika historia ya uanzishwaji wa kilimo cha mazao ya biashara barani Afrika licha ya ukweli kwamba hatua ya utawala wa kikoloni juu ya kutoa ruhusa rasmi kwa wazawa kulima mazao ya biashara ilipokelewa kwa hisia tofauti kulingana na eneo husika. Historia ya kuanzishwa kwa kilimo cha kahawa kwa

jamii ya Wachaga waishio mkoani Kilimanjaro na Wameru waishio kwenye miteremko ya Mlima Meru inaonyesha kutofautiana kwa maamuzi ya tawala za kikoloni.

2. Vigezo vya Kilimo cha Kahawa

Mbali na misingi ya historia ya ukoloni barani Afrika ambayo ni muhimu kuelezea, historia nzima ya kilimo cha kahawa kwa Wameru kama ilivyo kwa jamii nyingine, inategemea na vigezo vya jumla vya kilimo hicho ambavyo ni lazima kuvibainisha. Kwanza, ni kigezo cha hali ya hewa ambapo kilimo hicho kinaweza kufanyika tu katika eneo ambalo ardhi yake na hali ya hewa inaruhusu ukuaji wa zao lenyewe. Pili, ni lazima kilimo chenyewe kiwe na ufanisi kiuchumi na kiwe kimekubalika kisiasa. Na mwisho, ni ukweli ulio wazi kuwa kigezo cha utayari wa kibinadamu nacho kina umuhimu mkubwa.

2.1. Kigezo cha Hali ya Hewa

Aina mbili kuu za kahawa ambazo ni Arabica na Robusta, hazistawi katika hali ya hewa inayofanana bali kila moja hustawi kwenye hali ya hewa ya peke yake. Robusta huitaji maji mengi zaidi kuliko Arabica, na hivyo inastawi katika hali ya hewa ya ‘kiikweta’ yenye viwango vya juu vya joto na unyevu. Arabica yenyewe inaweza kustawi katika maeneo yenye viwango vya chini vya joto ambayo yanapatikana katika miinuko ya kati ya mita 1500 na 1900 kutoka usawa wa bahari, kama vile katika miteremko ya Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru. Mahitaji ya Robusta ndiyo yanaelezea sababu ya kulimwa kwake katika maeneo ya tambarare ya Magharibi na Kaskazini mwa Ziwa Victoria: Magharibi ni katika eneo

wanaloishi jamii ya Wahaya na Kaskazini ni kwa upande wa Uganda (Zwanenberg, R. M., 1975:70; Iliffe, J., 1979:281-).

Vigezo hivyo vilikuwa ndivyo sababu ya kushindwa kwa majaribio ya kwanza ya kilimo cha Arabica upande wa Tanganyika ambayo yalifanyika mwaka 1891 katika Milima ya Usambara. Arabica haikuweza kustawi kutokana na kiwango kikubwa cha tindikali katika ardhi na hali ya hewa ya ukavu na joto kali katika maeneo ya chini ya Milima ya Usambara huku kukiwa na baridi kali na unyevu unyevu mwingi katika miteremko yake ya upande wa magharibi (Iliffe, J., 1979: 126-128). Kinyume na ilivyokuwa katika Milima ya Usambara, majaribio yaliyofanyika katika maeneo ya pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro yalionyesha mafanikio makubwa ambapo Arabica iliweza kustawi vizuri hapo katika ardhi ya 'kivolkano' yenye rutuba na yenye kupata mvua ya kutosha kwa mwaka.

2.2. Kigezo cha Kiuchumi

Ili kilimo cha kahawa kiweze kufanikiwa katika maeneo ambayo yanaonekana yanafaa, ni lazima pia kuwepo na mazingira bora ya kiuchumi: mbinu za kilimo zenye kuhakikisha mavuno bora, kuwepo kwa nguvu kazi, usafirishaji wa uhakika, miundo mbinu thabiti, uhakika wa soko na bei nzuri ya bidhaa husika katika soko la dunia. Vigezo hivi vyote vilitimizwa katika historia ya ukuaji wa kilimo cha kahawa kwa Wameru. Wakulima wenyewe, kwa juhudi zao binafsi walijibidisha kutimiza kila kigezo kwa kadiri walivyoweza. Hata hivyo, wakati mwingine walikumbwa na changamoto ya kutokuwa na uwezo wa kutathmini kigezo kilicho muhimu zaidi ambacho ni kile cha uhakika wa soko la dunia la kahawa na bei ya kiridhisha.

2.3. Kigezo cha Kisiasa

Majaribio ya awali ya kahawa katika eneo la Afrika Mashariki yalitokana na kuwepo kwa soko zuri la kahawa duniani. Katika miaka ya 1870-1880, Uingereza ilikuwa ikiagiza kahawa yake kutoka Ceylan na India, lakini baada ya mwaka 1880, ugonjwa wa jani la kahawa uliangamiza mashamba ya kahawa ya Ceylan na hivyo Uingereza ikalazimika kuwa inaagiza kahawa yake kutoka Brazili ili kukidhi haja ya mahitaji ya soko lake la kahawa.

Wakati huo, Brazili ndiyo ilikuwa mzalishaji mkubwa wa kahawa duniani. Biashara ya zao hilo ilikuwa imehodhiwa na Marekani na hivyo mwishoni mwa mwaka 1890 bei yake iliongezeka sana. Uingereza, ambayo katika miaka michache nyuma ilikuwa ikijipatia faida kubwa kwa kuuza kahawa ya Ceylan katika soko la Ulaya, ikalazimika kutafuta maeneo ya kuzalisha bidhaa hiyo kutoka kwenye makoloni yake ambayo yalikuwa ni Afrika Mashariki. Hivyo kuanzia mwaka 1905, kilimo cha kahawa kilianza kuhimizwa kisiasa katika koloni la Uingereza la Kenya (Zwanenberg, R.M., 1975:186), ambapo majaribio kama hayo ya kulima kahawa katika koloni la Ujerumani la Tanganyika yalianza mwaka 1886 hadi 1914.

2.4. Kigezo cha Kibinadamu

Kigezo kinachohusiana na watu kilibeba umuhimu mkubwa katika uanzishwaji wa kilimo cha kahawa katika maeneo mengi ya Afrika Mashariki. Kahawa ya Arabika ambayo asili yake ni Ethiopia ilianza kulimwa katika karne za 14 na 15 lakini kutumika kwake kama kinywaji muhimu duniani hakukuanza siku nyingi sana. Kwanza kilimo chake kilianza

kuendelezwa na Waarabu na kisha Waholanzi wa Java katika karne ya 16. Barani Ulaya, mahitaji ya kahawa kama kinywaji muhimu yalianza kuongezeka katika karne ya 18 na hivyo kusababisha nchi za Ulaya kuhimiza kilimo hicho hususan katika nchi za Amerika ya Kusini na baadaye Afrika.

Mwishoni mwa karne ya 19, mashamba makubwa ya kwanza ya kahawa katika eneo la Afrika la Mashariki yalikuwa ni ya Wamisionari na Wakoloni wengine, na baadaye ndipo wazawa wakawaiga. Wamisionari hao ambao walikuwa wakijitahidi kueneza dini, waliweza kukubalika kwa wazawa kutokana na msimamo wao wa kuwaunga mkono wazawa katika harakati zao za kutaka kuruhusiwa kulima kahawa, tofauti na msimamo wa watawalawa Kikoloni ambao walitaka kahawa ibaki kuwa ni kilimo chao peke yao ili kuendelea kunufaika nayo wao wenyewe. Msimamo huo ulichangiwa pia na hofu ya kutopata vibarua katika mashamba yao endapo wazawa nao wangeruhusiwa kulima zao hilo. Aidha walitumia pia hoja kwamba Waafrika wangesababisha mashamba ya Wakoloni kuathiriwa na ugonjwa unaoshambulia miti ya kahawa kwa kuwa Waafrika hawana ujuzi thabiti wa kilimo hicho.

Hata hivyo, Wakoloni waliweza kudhibiti kilimo cha kahawa pale tu ambapo idadi yao iliwatosha kuweza kusimamia mashamba yao na hivyo kuweza kuzuia kabisa Waafrika kufanya kilimo hicho nchini Tanganyika, Kenya na Uganda. Hata hivyo, nchini Tanganyika Wakoloni walikuwa wachache pamoja na mgawanyo wake katika mikoa ulikuwa hauwiani ikilinganishwa na nchini Kenya. Wakoloni ni kama vile hawakuwepo kabisa katika maeneo ya jamii ya Wahaya

waishio magharibi ya Tanzania na hivyo kuwafanya Wahaya kuendeleza haraka kilimo cha kahawa aina ya Arabica na baadaye wakapata uungwaji mkono na Wakoloni wenyewe. Kuanzia mwaka 1928, mkulima mmoja wa Kihaya kati ya wawili alikuwa akilima kahawa. Katika kipindi hicho, kilimo cha kahawa ya Arabika miongoni mwa Wachaga mkoani Kilimanjaro kilikuwa bado hakijakua sana kwa kuwa idadi ya Wakoloni waliolima kahawa ilikuwa kubwa katika eneo hilo (Iliffe, J., 1979:281).

Kama tulivyoona hapo juu, Wakoloni wa Kijerumani na baadaye wale wa Kiingereza walioikalia nchi ya Tanganyika walitofautiana katika namna ya kuwazuia wazawa wasilime kahawa. Katika kutetea maslahi ya maendeleo ya wazawa, wapo watawala wa Kikoloni na Wamisionari waliosimama upande wa Waafrika. Msimamo huo wa Kanisa ulichangia sana kukubalika na kuenea kwa Ukristo katika Afrika Mashariki kama ilivyo kwa Wameru.

Wakulima wa kwanza wa kahawa wa Kiafrika walikuwa ni wale ambao walipata fursa ya kuwa na mahusiano na Wazungu wakiwemo Wamisionari. Kwa upande wa vibarua wa Kiafrika katika mashamba ya Wazungu, wao hawakuweza kuanzisha kilimo hicho katika mashamba yao wenyewe kwa sababu hawakuwa na muda na pia Waajiri wao hawakuwaruhusu kuondoka na miche ya kahawa. Hivyo, ni wale Waafrika wa kwanza walioingia katika Ukristo ndio ambao walikuwa wa mwanzo katika kuanzisha kilimo cha kahawa katika mashamba yao japo watoto wa Kiafrika waliokuwa wakisoma katika Shule za Wamisionari walipaswa kufanya kazi katika mashamba ya kahawa ya Wamisionari hao ambao mbali na kulima kahawa

walikuwa wanalima pia mazao ya chakula. Watoto hao wa Shule walijifunza kilimo cha kahawa na baadaye waliweza kuanzisha na kuendesha kilimo hicho katika mashamba ya wazazi wao.

3. Kilimo cha Kahawa Kaskazini mwa Tanzania

Kukua na kuendelea kwa kilimo cha kahawa kwa wazawa wa Kaskazini mwa Tanzania katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro na Magharibi mwa Mlima Meru kunahusianishwa moja kwa moja na kukua kwa Injili katika maeneo hayo. Kuenea huku kwa kahawa kulianza mapema kwa Wachaga huko Kilimanjaro kwa kuwa mwingiliano wao na Wamisionari wa Kizungu ulianza mapema zaidi kuliko ilivyokuwa kwa Wameru. Kwa hiyo, kuna haja hapa ya kueleza kwanza kwa ufupi historia ya kilimo cha kahawa katika jamii ya Wachaga. Historia hiyo imeandikwa vizuri na J. Iliffe (1979) na S. F. Moore (1977 na 1986).

Kupungua kwa bei ya kahawa katika soko la dunia wanzoni mwa karne ya 20 kulisababisha kusimama kwa majaribio ya ya kwanza ya zao la kahawa katika ya Milima ya Usambara. Kuimarika tena kwa bei hiyo katika soko la dunia mnamo mwaka 1910 kuliwafanya Wakoloni kuongeza kilimo hicho katika eneo jipya ambalo ni la katika Milima ya Kilimanjaro na Meru. Shamba kubwa la kwanza la kahawa katika maeneo hayo ambayo majaribio yalionyesha kuwa yanafaa kwa kahawa ya arabika, lilikuwa limeshaanzishwa tangu mwaka 1894 (Iliffe, J., 1979:126-128 na 143-144; Moore, S. F., 1986:103).

Vigezo mbalimbali vya kiuchumi na kijamii vilichangia katika kutofautiana kwa historia ya kilimo cha kahawa baina ya maeneo hayo mawili ya Meru na Kilimanjaro licha ya kwamba yote yalikuwa na hali ya hewa inayofaa kwa kilimo hicho. Kahawa iliendelezwa haraka zaidi Mkoani Kilimanjaro. Katika kipindi cha karne za 18 na 19, Kilimanjaro ilikuwa kitovu cha biashara ya pembe za ndovu na watumwa (Moore, S., 1997:7-15) wakati Wameru waliopo upande wa Magharibi hawakujihusha kabisa na biashara hizo. Baadaye, waeneeza Injili wa Kizungu walifika Kilimanjaro ambapo Wamisionari wa kwanza walifika mwaka 1885 wakati katika jamii ya Wameru, Wamisionari walifika tena na kufanikiwa kuanza kazi yao mnamo mwaka 1902 ikiwa ni miaka 17 baada ya wale waliofika Kilimanjaro. Ni wazi kuwa kuuawa kwa Wamisionari wawili wa kwanza katika eneo la Meru mwaka 1896 kulichelewesha majaribio mapya ya Wamisionari kwenda kueneza Ukristo katika eneo hilo.

Kutokana na kujiingiza mapema katika biashara za masafa marefu, Wachaga waliweza kujipatia nyenzo na mbinu za kisasa za usafirishaji wa kahawa mapema zaidi kuliko Wameru. Mwaka 1912 wakati wa Ukoloni wa Wajerumani, njia ya reli inayounganisha Moshi na Pwani ilikamilika kujengwa na hivyo kutoa uhakika na urahisi wa usafirishaji wa kahawa. Ni hadi mwaka 1929, chini ya utawala wa Waingereza, ndipo reli hiyo ilipoendelezwa hadi katika kijiji cha Tengeru kilicho chini ya Mlima Meru, ikiwa ni miaka 17 tangu kukamilika kwa reli hiyo kule Moshi. Mwaka mmoja baadaye, reli hiyo iliendelezwa kwa umbali wa kilomita 13 kwa upande wa magharibi hadi kufikia huko Arusha mjini. Vigezo hivi vya kuanza mapema kwa

ulimaji wa kahawa chini ya ushawishi wa Wamisionari pamoja na miundombinu imara huko Kilimanjaro vilichochea ustawi mzuri na wa mapema wa kahawa kwa Wachaga kulinganisha na Wameru.

Kigezo kingine kilichofanya kilimo cha kahawa kuenea haraka Mkoani Kilimanjaro ni ukweli kwamba mashamba ya Wakoloni hayakuwa mengi sana na hivyo hakukuwa na unyan'ganyaji mkubwa wa ardhi kwa wazawa (Iliffe, J., 1979:144). Wameru kwa umoja wao walijitahidi sana kudhibiti ardhi yao isichukuliwe na wageni, hata hivyo Mlima Meru ulikuwa umezingirwa na mashamba makubwa ya Wakoloni kwa upande wa kusini na mashariki (Luanda, N. N., 1986:51). Kutokana na wingi wao pembezoni mwa Mlima Meru, wakulima wa Kikoloni walikuwa na ushawishi mkubwa zaidi kwa watawala wa Kikoloni. Kwa upande mwingine pia, ni kwamba baada ya Vita ya Pili ya Dunia, Wachaga walinufaika na msaada mkubwa uliofanywa na Afisa Tawala wa kwanza kabisa, Meja Charles Dundas. Wachaga wengi walikuwa tayari wanalima kahawa kwa wakati huo (miti 125,000 ya kahawa ilikuwepo tayari kwa Wachaga mnamo mwaka 1921) japo walikuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya soko la kuiuza. Dundas na kisha Afisa mwingine aliyefuata waliwezesha kuanzishwa kwa chama cha kwanza cha ushirika wa biashara ya kahawa cha Wachaga (KNPA) kilichoanzishwa mwaka 1925 (Moore, S. F., 1986:119).

Wachaga walikuwa na bidii sana kwa maendeleo yao ambapo kwa jitihada zao wenyewe walitengeneza barabara hasa sehemu za mlimani ili kurahisisha usafirishaji wa kahawa yao. Wachaga pia walisaidiwa sana na sera ya Wakoloni ya

kuhimiza kilimo cha kahawa licha ya kuwepo kwa upinzani mkali kutoka kwa wakulima wakubwa wa Kizungu wa Kenya na Tanganyika. J. Iliffe ameandika kwa kina mabadiliko ya kijamii yaliyotokana na kuanzishwa kwa kilimo cha kahawa katika jamii ya Wachaga, hususan kujitokeza kwa tabaka tajiri dhidi ya viogozi wa kijadi na kuibuka kwa uelewa wa kisiasa (J. Iliffe 1979:274-281).

Hata hivyo, kitabu cha Iliffe hakielezi kwa kina historia ya kilimo cha kahawa kwa Wameru ambayo inaelezwa katika vitabu vingine, kama vile, andiko la utafiti la N. N. Luanda, *European Commercial Farming and its Impact on the Meru and Arusha peoples of Tanzania, 1920-1955*, tafiti za mwanajamii P. Puritt (1970 na 1977), historia ya maisha ya mmoja wa Walutheri wa kwanza Meru, Mathayo Kaaya, zilizochapishwa na A. S. Mbise (1973) pamoja na kazi murua ya Mmarekani A. Nelson (1967) ambaye aliletwa na Wameru katika miaka ya 1950 kwa ajili ya kuwasaidia kuendeleza kilimo cha kahawa. Kadhalika, simulizi za mdomo ni muhimu sana katika kueleza historia hiyo lakini havijatumika vya kutosha kwa kuwa utafiti katika jamii ya Wameru ulifanywa zaidi katika maeneo mengine ya utoaji habari.

4. Kilimo cha Kahawa kwa Wameru

Ikilinganishwa na mkoani Kilimanjaro, kilimo cha kahawa kwa Wameru kilichelewa kutokana na kuchelewa kupokelewa kwa Wamisioanri walioeneza Injili, kuchelewa kwa ujenzi wa miundo-mbinu ya usafirishaji pamoja na uwepo mkubwa wa Wakoloni wa Kizungu katika eneo la Mlima Meru. Eneo la chini

ya Mlima Meru liligeuka kuwa eneo la Wazungu ambapo hekta 37, 720 zilikuwa zimechukuliwa na Wazungu kufikia mwaka 1910 (Iliffe, J., 1979:145) na hekta 45, 608 kufikia mwaka 1925 (Luanda, N.N., 1986:80).

4.1. Mwanzo wa Kilimo cha Kahawa

Kuanzia mwaka 1906, ikiwa ni miaka minne tangu kuanzishwa kwa kituo cha kwanza cha Umisioni wa Kilutheri kwa Wameru kule Nkoaranga, Wameru wa kwanza waliojiunga na Ukristo walianza kulima kahawa katika mashamba yao kutokana na mimea iliyotolewa kwa wanafunzi wa Shule ya Wamisionari walioichukua kwa lengo kuwa wanaenda kutengeneza kahawa kwa matumizi ya kunywa. Ukweli ni kwamba, unywaji wa kahawa haukuwahi kuwa desturi muhimu kwa Wameru hadi hivi sasa. Kwa Wameru, kahawa siyo zao la kulilima peke yake na hata Wameru wa kwanza kulima kahawa walikuwa wakizalisha kiwango kidogo kwa kuchanganya na mazao mengine. Mikahawa, ambayo ililimwa pamoja na migomba, mahindi na maharagwe, kwanza ilipandwa kwa kuficha ili wakoloni wasijue na baadaye upinzani ulikuwa mkali zaidi dhidi ya kilimo hicho. Pamoja na vikwazo hivyo, wakulima wa Kimeru pia walikabiliwa na changamoto ya kukosa miundo-mbinu ya kibiashara.

Mathayo Kaaya ambaye ni mmoja wa Wameru wa kwanza kuingia katika Ukristo mwanzoni mwa karne ya 20 na ambaye historia yake imeandikwa na Bwn. A. S. Mbise (1973), alieleza hali ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya 1920. Kwa mujibu wake, idadi ya watu katika jamii ya Wameru kwa wakati huo ilikuwa ndogo: takribani watu 12,000 (Spear 1993:135). Katika kuuza kahawa yao, Wameru walisaidiwa na Wamisionari

wawili wa Kijerumani ambao walibaki baada ya Vita ya Kwanza ya Dunia. Vile vile, Wakuu wa Wilaya wa mwanzoni nao pia waliwasaidia Wameru kuuza kahawa yao kwa wafanyabiashara wakubwa wa Kizungu na Kihindi mjini Arusha (Mbise, A. S., 1973:39).

Kama anavyoeleza Luanda, kulikuwa na tofauti ni kubwa ya ufanisi wa kilimo cha kahawa kati ya Wachaga na Wameru. Kwa Wachaga, kuanzishwa chama cha ushirika cha K.N.P.A mwaka 1924, kulisaidia sana. Kilikuwa ni taasisi kubwa ya kibiashara ambayo ilijihusisha na mambo mengi kuanzia usajili wa mashamba ya kahawa kwa utawala, ununuzi na usambazaji wa dawa za wadudu, na vifaa vingine kwa ajili ya kilimo cha kahawa na hadi mauzo ya kahawa yenyewe. Wakulima wote wa kahawa mkoani Kilimanjaro walikuwa wanachama wa chama hicho cha kipekee.

Kinyume chake, kwa Wameru, haikuwa lazima kujiunga na chama cha ushirika. Kila mkulima alifanya mwenyewe usajili wa shamba lake pamoja na kuuza kahawa yake mwenyewe kwa wafanya-biashara anaowataka yeye mwenyewe. Kutokana na kukosekana kwa bei ya pamoja, bei yao ya mauzo ya kahawa ikawa ndogo sana. Mwaka 1928, Wameru waliunda chama cha ushirika na majirani zao wa jamii ya Waarusha walioko katika miteremko ya kusini-magharibi mwa Mlima Meru. Lakini mwaka 1931 ushirika huo ulivunjika. Kati ya mwaka 1929 na 1930 Wameru walipata wakala wa kuuza kahawa yao mjini London, Uingereza; lakini hawakuweza kunufaika sana kwani ilionekana kuwa kahawa yao haikuwa na kiwango bora na hivyo kukasababisha kuporomoka kwa bei ya zao la kahawa ambapo malipo ya awali yaliyolipwa na wakala

huyo kwa wakulima hayakutosha hata kufidia gharama za kuosha na kusafirisha kahawa yao. Chama chao cha ushirika kilipata hasara na kesi ikaamuliwa mahakamani (Luanda, N. N., 1986:161-163, 173).

Kiwango duni cha ubora wa kahawa ndiyo moja ya sababu za matatizo hasa ya kuporomoka kwa bei yake. Kabla ya mwaka 1934, Wameru walikuwa hawaweki mbolea wala kupuliza dawa ya wadudu katika miti yao ya kahawa ambayo pia ilikuwa haikatiwi, jambo ambalo lilikuwa lilisababisha mimea hiyo kushambuliwa na wadudu na magonjwa. Kuanzia mwaka 1922, kushambuliwa kwa mikahawa katika mashamba makubwa ya kahawa ilikuwa ni tatizo sugu. Mwaka 1934, kitengo cha kilimo cha mkoa wa Arusha, kiliendesha zoezi la kuharibu miti 37,000 ya kahawa iliyokuwa imeathiriwa na magonjwa ya kahawa katika ardhi ya Wameru na miti 75,000 katika ardhi ya Waarusha. Licha ya kwamba zoezi hilo halikueleweka vizuri kwa wazawa lakini kuanzia kipindi hicho dawa za wadudu wa kahawa zilianza kutumika kwa mara ya kwanza. Kabla ya kipindi hicho, mbinu zilizokuwa zikitumika kuzuia maradhi dhidi ya kahawa zilikuwa hafifu: vikundi vya watoto vilikuwa vikiundwa kwa ajili ya kuwaondoa wadudu kwa kutumia mikono katika mashamba ya wakoloni na yale ya wazawa (Luanda, N. N., 1986:129-131 na 160).

Pamoja na kwamba hali ya usalama wa magonjwa kwa mikahawa ya wazawa haikuwa ya kuridhisha, hatari hiyo ilikumba pia mashamba ya Wakoloni kwani nayo yalikuwa hatarini kuambukizwa magonjwa ya mimea hiyo. Hali hiyo ya maambukizi ya magonjwa ya kahawa ndiyo ilitolewa na wakulima wakubwa wa Kikoloni katika kuwazuia wakulima wa

Kiafrika kulima zao hilo japo haikuwa sababu pekee ya kuwazuia Waafrika kufanya kilimo hicho. Hofu nyingine ya Wakoloni hao ilikuwa ni kukosa vibarua wa kulima katika mashamba yao kwa kuwa tayari Wameru walikuwa wakipinga kufanya kazi hizo za vibarua. Ni wanawake na watoto ndiyo waliokuwa wakitumiwa zaidi kufanya kazi ya vibarau kwa Wakoloni hususan wakati wa mavuno kwa makubaliano ya kuruhusiwa kutumia vyanzo vya maji kwa kuwa mashamba mengi ya Wazungu yalikuwa katika eneo la chini la Mlima Meru ambalo pia ndilo eneo lililokuwa na vyanzo vya maji. Suala hilo la vyanzo vya maji kuwa ndani ya maeneo ya Wazungu lilikuwa kikwazo kikubwa kwa wazawa katika kunywesha mifugo yao. Hivyo Wameru walikuwa wakifanya vibarua vya muda tu katika mashamba ya Wazungu na wakati mwingine bila ya malipo. Asilimia kubwa ya vibarua katika mashamba hayo walikuja kutoka mbali hususan maeneo ya kati mwa Tanganyika.

Miongoni mwa sababu zilizotolewa na Wakoloni ili kuuchochea utawala kuwazuia Waafrika kulima kahawa, ni wazi kuwa hofu ya ushindani ndiyo ilikuwa sababu kubwa zaidi. Mwaka 1926, shinikizo la wakulima wakubwa wa Kizungu ndilo lililoufanya utawala wa Kikoloni kujaribu kuwakatisha tamaa Wameru na Waarusha kulima kahawa ya arabika lakini bila ya mafanikio (Iliffe, J., 1979:289-290). Mgogoro baina ya wakulima wa kikoloni na Wameru ukawa mkubwa kiasi ambacho Wameru walimtuhumu kiongozi wao wa kijadi kuwa alikuwa amehongwa na upande wa Wakoloni kwani alishindwa kuwatetea (Mbise, A. S., 1973:39). Wakulima wa Kizungu wa Wilaya ya Arusha, chini ya Chama cha Wakulima wa Kahawa

Arusha (Arusha Coffee Planters' Association), walikubaliana na kupitisha azimio la kupiga marufuku kilimo cha kahawa kwa Waafrika kati ya mwaka 1924 na 1927, azimio ambalo halikufanikiwa, na kufikia mwaka 1936 walitupilia mbali azimio hilo na badala yake walisisitiza kuwepo kwa usalama wa mashamba yao ya kahawa dhidi ya magonjwa hatari ya kahawa yaliyoonekana katika mashamba ya wazawa (Luanda, N. N., 1986:174-179).

Kuanzia mwaka 1929, kutokana na mgogoro wa kiuchumi duniani, kuporomoka kwa bei ya kahawa kuliwaathiri vibaya sana wakulima wa kahawa wa mkoani Kilimanjaro ambao zao hilo lilikuwa ni chanzo kikubwa cha mapato. Lakini katika mkoa wa Arusha ambapo kilimo hicho bado kilikuwa kichanga, mtikisiko huo wa uchumi wa dunia haukuwa na madhara makubwa sana. Kilimo cha kahawa kilikuwa na mchango mdogo katika uchumi wa watu wa Arusha na kiliendelea kukua taratibu ambapo kipato cha familia kilitegemea pia kilimo cha mazao ya chakula (ndizi, mahindi na maharagwe). Mwaka 1930, Wilaya ya Arusha (ambayo ilijumuisha Wameru na Waarusha) ilikuwa na mashamba 400 tu ya kahawa. Miaka mitano baadaye, mashamba hayo yalifikia 1,300 katika eneo la ukubwa wa hekta 31. Mwaka 1935, serikali ya Kikoloni ilipinga tena vikali kilimo cha kahawa kwa Waafrika (Nelson, A., 1967:107), na kukifanya kilimo hicho kiwe hafifu kwa Wameru. Mwaka 1938 Mmeru mmoja tu kati ya wanne ndiye aliyekuwa akilima kahawa (Iliffe, J., 1979:293). Katika kipindi hicho Wameru bado hawakuwa na muungano wao, na hakukuwa na mpangilio maalum na imara wa kibiashara.

4.2. Mabadiliko Muhimu Miaka ya 1950

Mabadiliko makubwa yalijitokeza kuanzia miaka ya 1947-1952, kipindi ambacho ni muhimu sana katika historia ya Wameru. Idadi ya Wameru ilikuwa imeongezeka kwa takribani mara mbili katika kipindi cha miaka 30 na kufikia kiasi cha watu wapatao 30,000. Kipindi hicho pia kilikumbwa, mara mbili, na juhudi za utawala wa Wakoloni kukwamisha juhudi za wazawa kulima na kuuza kahawa.

Juhudi za utawala wa Kikoloni za kukwamisha kilimo cha kahawa kwa wazawa zilianza kwa kuchapishwa kwa ripoti ya Wilson iliyopendekeza kuchukuliwa kwa ardhi ya mifugo ya Wameru upande wa kaskazini mashariki mwa Mlima Meru na kisha ardhi hiyo kupewa wakulima wa Kikoloni. Ripoti hiyo ilipendekeza pia kuhamishwa kwa Wameru waishio katika ukanda huo kuelekea eneo kame la King'ori ambalo kwa wakati huo lilikuwa bado halina watu wakioishi huko. Wameru walikataa kukandamizwa na Wakoloni na ndipo walianza harakati zao za upinzani zilioongozwa na wasomi wa kwanza wa Kilutheri, harakati ambazo ni maarufu katika historia ya Tanganyika na zinazojulikana kama Meru Land Case.

Baada ya mvutano, mgogoro huo ulifikia hatua yake kubwa kabisa mwaka 1952 baada ya Wameru kumtuma nchini Marekani mwakilishi wao Bwana Kirilo Japheti kupeleka malalamiko yao Umoja wa Mataifa juu ya kuporwa ardhi yao na Wakoloni. Baada ya Vita kuu ya Pili ya Dunia, Jumuiya ya Mataifa ambayo baadaye ilikuja kuwa Umoja wa Mataifa (UN) iliiweka Tanganyika chini ya uangalizi wa Uingereza mwaka 1946, na Kirilo Japhet akaalikwa kutetea ombi la watu wake mbele ya Baraza la Utawala la Umoja wa Mataifa tarehe 21

Julai 1952. Utetezi huo umebaki kuwa jambo la kujivunia sana kwa Wameru kwa kuwa ilikuwa ni kwa mara ya kwanza jamii ndogo ya watu wasiojulikana kimataifa na walio chini ya utawala wa Kikoloni kutetea tatizo lao mbele ya Baraza la Umoja wa Mataifa. Safari yenyewe ya Krilo Japhet kwenda nchini Marekani ilitokana moja kwa moja na sababu za kuendelea kwa kilimo cha kahawa kama ambavyo tutaona baadaye.

Kikwazo cha kibiashara kutoka kwa utawala wa Kikoloni kuanzia mwaka 1947 kinakigusa kilimo cha kahawa moja kwa moja. Wakoloni walipendekeza kwa Wameru kuunda Bodi ya Wazawa ya Kahawa Arusha (Arusha Native Coffee Board) ambapo wakulima wote watakuwa wakiuza kahawa yao. Kiongozi wa bodi hiyo atateuliwa na Mkuu wa Wilaya. Kwa kipindi hicho, uzalishaji wa kahawa kwa wakulima hao wa Arusha ulikuwa ni tani 200 kwa mwaka. Hata hivyo Wameru waliupinga mpango huo na kuisusia bodi hiyo. Badala yake, mwaka 1954, ikiwa ni miaka 7 baadaye, walikuja kulazimishwa kuufuata mfumo huo (Nelson, A., 1967:92, 134) ingawa kwa muda mfupi.

Kwa hakika, miaka ya 1950 ilikuwa ni ya mabadiliko makubwa katika historia ya Wameru na jamii zinazowazunguka. Mwaka 1952 kulitokea mapigano ya Mau-Mau nchini Kenya ambapo Wameru walifahamu kwa kina juu ya upinzani huo wa Wakenya dhidi ya Wakoloni. Miaka miwili baadaye, mwaka 1954, kiliundwa chama cha Tanganyika African National Union (TANU) ambacho ndicho kilikuwa chama thabiti kilichoanzisha mapambano ya kudai uhuru wa Tanganyika. Kirilo Japhet baada ya kuwasilisha tatizo la ardhi la

Wameru alibakia kwa muda kidogo nchini Marekani ambapo alikuwa akionana na kufanya mazungumzo na Walutheri wa nchini humo na ndipo akakutana na Anthon Nelson, kijana wa Kimarekani mwenye fikra za kijamaa ambaye alikuwa na ujuzi wa wastani wa ujenzi na biashara. Kirilo Japhet alimwomba warejee wote Tanganyika ili aje kuwasaidia Wameru katika kuendeleza kilimo chao cha kahawa ambapo angelipwa ujira wa wastani.

Anthon Nelson na Kirilo Japhet waliwasili kwa Wameru mwaka 1954. Baada ya muda mfupi Anthon Nelson akafahamu madhaifu yaliyoathiri kilimo hicho cha kahawa: tija hafifu kutokana na kuzalisha kahawa isiyo na ubora na hivyo kuishia kupata bei ya chini ya mauzo ya zao hilo. Hatua ya kwanza aliyoichukua Anthon Nelson ni kujadili uwezekano wa kupunguzwa kwa kodi inayotozwa na Wakoloni kwa mauzo ya kahawa sanjari na gharama ya wakala wa kahawa: kwa kipindi hicho, kodi ya kahawa ilikuwa asilimia 2.5 kwa Wameru huku wakulima wa Kikoloni wakilipa asilimia 1.5 tu, na gharama ya wakala ambaye alikuwa Moshi ilikuwa ni asilimia 1.5 kwa Wameru badala ya asilimia 1 tu iliyokuwa inatozwa kwa wakulima wasio Waafrika. Anthon Nelson aligundua kuwa ili kuwa na viwango vya chini vya tozo la kodi ilibidi waanzishe chama rasmi cha ushirika (Nelson, A., 1967:93-96).

Chama hicho, ambacho kiliitwa Meru Growers Cooperative Society, kilianzishwa mwaka 1955 na kuchukua nafasi ya Meru Coffee Growers Association kilichoanzishwa mwaka 1947 (Puritt, P., 1977:105) lakini hakikuwa na hadhi rasmi ya kushughulikia maslai ya Wameru. Chama hicho kipya cha ushirika kiliundwa kwa kufuata misingi ya kile cha

Wachaga, Kilimanjaro Native Cooperative Union (K.N.C.U.) ambacho kilianzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1930 kikichukua nafasi ya chama chao cha kwanza kilichoanzishwa mwezi Januari 1925 (Iliffe, J., 1979:277-279). Hivyo Wameru walichelewa kwa zaidi ya miaka 20 kuanzisha chama chao rasmi ikilinganishwa na majirani zao Wachaga.

Hatua alizochukua Anthon Nelson zilihusisha pia kuchagua miche bora na kupambana na wadudu wanaoshambulia kahawa. Katika miezi ya mwanzo ya kazi yake, mwaka 1955, alipata miche mizuri kutoka katika kituo cha utafiti cha Lyamungu huko Kilimanjaro. Aliisambaza kwa Wameru pamoja na kuwaelekeza matumizi ya dawa za wadudu wa kahawa na katika kipindi cha miaka mitano tu, tangu mwaka 1954 hadi 1959, mavuno ya kahawa kwa Wameru yaliongezeka kwa mara tatu au nne zaidi. Kinyume na kuporomoka kwa uzalishaji mnamo mwaka 1952, mavuno yao sasa yakafikia tani 500 mnamo mwaka 1958 na tani 830 mnamo mwaka 1960 (Nelson, A., 1967:107-110, 134).

Kwa wakati huo, Wameru pia walikuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa elimu ambapo mwaka 1954, kati ya jamii yenye watu 35, 000, ni wanafunzi wawili tu ndiyo walikuwa wamesoma hadi elimu ya sekondari. Kwa kuliona tatizo hilo, kwa kutumia fedha zake yenyewe, Kamati Kuu ya Chama cha Ushirika ikaanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kutilia mkazo maendeleo ya elimu. Mfuko huo ulitengewa nusu ya mapato ya chama ambayo ni asilimia 2 kati ya asilimia 4 ya kamisheni waliyotozwa wakulima wa kahawa wa Kimeru. Wakati huo huo, Kanisa la Kilutheri, ambalo ushawishi wake uliongezeka zaidi wakati wa Meru Land Case, walichangia

juhudi hizo za kukuza elimu kwa kuanzisha shule ya kwanza ya sekondari Meru iitwayo Shule ya Sekondari Makumira. Mwaka 1959, Anton Nelson kwa upande wake, hususan kutokana na uhusiano wake na watu wa Marekani, aliwezesha kupatikana kwa udhamini wa mwanafunzi wa kwanza Mmeru kwenda kuendelea na elimu ya juu katika chuo cha Kilutheri cha Minnesota, Marekani. Ni chama cha ushirika cha kahawa ndicho kilichogharamia safari ya mwanafunzi huyo (Nelson, A., 1967:146-150).

Mwaka 1958, uzalishaji wa kahawa kwa Wameru ulikuwa mkubwa sana kiasi cha kukizidi uwezo chama chao cha Meru Growers Cooperative Society na hivyo chama hicho kubadilishwa na kuwa ushirika wa vyama vya ushirika Meru na kikaitwa Meru Cooperatives Union. Ushirika huo ulinunua na kuuza karibu kahawa yote iliyozalishwa na wazawa. Pamoja na kupungua kwa soko la dunia, uzalishaji uliimarika zaidi kwa idadi na kwa ubora ambapo mapato ya zao hilo yaliongezeka sana. Utajiri wa ushirika huo ukawezesha kuyanunua na kuyagawa upya mashamba ya Wazungu moja baada ya jingine, mashamba ambayo yalichukuliwa kinguvu na Wazungu na kisha kuyatelekeza wakati wa Meru Land Case (Nelson, A., 1967:133-134 na 152-153).

Kwa msaada wa Anthon Nelson, miundombinu ya usafiri katika eneo la Meru nayo ilikuwa imeimarika sana kufikia mwishoni mwa miaka ya 1950. Madaraja yalikuwa yamejengwa baina ya mito na mifereji mingi inayoshuka kutoka mlimani. Ujenzi huo ulihusisha pia ujenzi wa miundombinu ya kukusanya maji kwa ajili ya kuosha kahawa. Mradi wa maji wa kijiji cha Songoro, ambao ulikamilika mwaka

1959, ulikuwa unatega maji kutoka katika chanzo cha chemchem na kuyapeleka katika kiwanda cha Ngyani ambacho ndicho kilikuwa kiwanda cha kwanza cha kuchambua kahawa cha Wameru chini ya Umoja wao wa vyama vya Ushirika.

Hazina kubwa iliyotokana na kilimo cha kahawa katika kipidi cha kati ya mwaka 1950 na 1960 iliwawezesha Wameru kuwa na utajiri mwinig na wa kutosha. Sehemu kubwa ya utajiri huo iliwekezwa katika ufugaji na elimu. Hata hivyo, kukua kwa kilimo cha kahawa na kuongezeka kwa idadi ya watu, (idadi ya Wameru kwa mwaka 1960 ilifikia watu 50, 000), kulisababisha uhaba wa ardhi hasa kutokana na Wameru kuyageuza mashamba yao ya zamani kuwa mashamba ya kahawa na kwenda kuishi katika maeneo ambayo awali hayakuwa na makazi mengi ya watu. Kidogo kidogo, maeneo ya jirani yakaanza kupata wakazi kama vile ukanda wa malisho wa kaskazini mashariki mwa Mlima Meru, mbuga ya Mbuguni iliyopo upande wa kusini ambao hadi wakati huo hakukuwa na watu, pamoja na eneo la King'ori lililopo upande wa mashariki mwa Meru. Katikati ya miaka ya 1960, karibu kila mkulima wa Kimeru alilima kwa uchache heka moja ya kahawa ambayo ni sawa na ukubwa wa miche ya kahawa ipatayo 50 hadi 100 (Puritt, P., 1977:96).

Mwaka 1961, Tanganyika ilipata uhuru wake na taasisi na mipango ya maendeleo ikaanza rasmi kiserikali. Mara moja, Wizara ya Maendeleo ya Ushirika ikawaambia Wameru: "Kwa nini mtumie gharama kumlipa mtaalamu wa kilimo wakati ambapo mkiomba tu mnaweza kumpata mtaalamu bila ya kulipa chochote?" (Nelson, A., 1967:213). Hapa ndipo Anthon Nelson aliposhukuriwa na kuondoka Meru, ikiwa ni baada ya

miaka 7 ya huduma yake kwa Wameru. Habari zake zimeandiwa kwa kina katika Kitabu cha 'The Freemen of Meru' kinachosimulia uzoefu na huduma yake na ambacho kinamalizia kwa kusisimua sherehe aliyoandaliwa na Wameru mnamo mwaka 1962 katika kuadhimisha miaka 10 ya Meru Land Case.

HITIMISHO

Katika ardhi yenye rutuba ya miteremko ya Mlima Meru ambayo inafaa kwa kilimo cha kahawa, ni vigezo vya utayari wa kibinadamu ndivyo vilivyokuwa na uzito katika kila kipindi cha historia ya kilimo hicho kuanzia kuanzishwa kwake kwa kuchelewa tofauti na Mkoani Kilimanjaro, kasi yake ndogo ya ukuaji ambayo inahusishwa na ugumu wa kujipanga kwa wakulima wa kahawa wa Kimeru, hadi kushamiri kwake katika miaka ya 1960.

Miongoni mwa vigezo hivyo vya utayari wa kibinadamu tunaona tangu mwanzo, kazi ya Kanisa la Kilutheri. Ni Wamisionari wa kwanza wa Kilutheri ndio walioanzisha kilimo cha kahawa kwa Wameru na kuwasaidia kuuza zao hilo tofauti na wakulima wahamiaji wa Kizungu. Kwa hivyo historia ya kilimo cha kahawa katika miteremko ya Mlima Meru kama ilivyo huko Mlima Kilimanjaro, inahusiana sana na historia ya Ukristo katika maeneo hayo.

Kuchelewa kuanza kwa kilimo cha kahawa na ugumu uliyokumbana nao (matatizo ya magonjwa ya kahawa, vikwazo kutoka kwa wakulima wa Kizungu, ugumu wa kuuza zao lenyewe) viliwasilishwa na matakwa ya kibinadamu. Kutokana

na hali hiyo, Wameru walichelewa kuanza kilimo hicho, ikilinganishwa na Wachaga ambao wao walikabiliana na ugumu kama huo mapema. Mbali na kutofautiana katika kasi ya kuenea kwa Ukristo, kuimarika kwa miundombinu na kukua kwa elimu ambavyo pia ni vigezo muhimu, tofauti nyingine muhimu baina ya jamii hizo mbili ilikuwa ni vigezo vya kiuchumi na kijamii. Wachaga walionyesha mapema ufanisi hususan katika kuunda umoja wa jumla katika kilimo cha kahawa wakati Wameru wao walianza zaidi kwa mtindo wa kila mtu peke yake, mtindo ambao sababu zake zinaonekana ngumu kuzichambua.

Katika miaka ya 1950, majaribio ya Wakoloni kutaka kuchukua ardhi ya wazawa katika Meru yalisababisha, kupitia Meru Land Case, kuibuka kwa hisia kali za umoja miongoni mwa Wameru na hivyo kusababisha safari ya Kirilo Japhet nchini Marekani ambayo kwa ujumla ilikuwa ya mafanikio sana. Katika simulizi ya safari ya Kirilo Japhet na kurejea kwake akiwa na Mmarekani Anthon Nelson, tunaona pia kuhusika kwa Kanisa la Kilutheri. Kijana huyo msomi aliyeteuliwa na jamii yake kwenda kutetea tatizo lao mbele ya jumuiya ya Kimataifa naye ni Mlutheri, jambo hili halikutokea kwa bahati bali ni kutokana na ukweli kwamba wasomi wa kwanza walikuwa ni wanafunzi wa Wamisionari wa Kilutheri. Akiwa nchini Marekani, Kirilo Japhet alikuwa karibu sana na Walutheri, na kupitia Walutheri hao, aliweza kukutana na Anthon Nelson, mtaalam wa kilimo ambaye alirejea naye Meru. Kuja kwa Anthon Nelson, ambako kulikuwa ni matakwa ya Wameru ambao pia ndio waliomlipa, kulisababisha ustawi wa haraka wa kilimo cha kahawa.

Umuhimu wa Kanisa la Kilutheri katika ukuaji wa kilimo cha kahawa siyo kitu kigeni: tunauona pia katika historia ya ukuaji wa zao la kakao katika nchi tatu za Afrika Magharibi kama zinavyoelezwa katika kitabu cha J.-P. Chauveau. Kwa ujumla, utafiti zaidi unahitajika juu ya ushawishi wa Walutheri katika nyanja za kiuchumi katika nchi za Kiafrika ambapo Walutheri wana waumini wengi.

Hali ya kukua kwa kilimo cha kahawa kwa Wameru kati ya mwaka 1950 na 1960 iliambatana na hali ilivyokuwa nchini Kenya kufuatia mpango wa Swynnerton kuanzia mwaka 1953 (Adam, M., 1994:73-74). Mbali na kigezo cha utayari wa watu, kukua na kustawi kwa kilimo cha kahawa kulitegemea pia historia ya utawala wa wakati husika. Kwa kiasi kikubwa, kufanikiwa kwa kilimo cha kahawa kwa Wameru hakukutokana tu na umahiri wa mtaalamu mshauri aliyeletwa na Wameru, bali pia kulichochewa kwa kiasi kikubwa na azma ya kweli ya Wameru wenyewe katika kilimo hicho.

VITABU VYA REJEA

ADAM, M., 1994, Une revanche post-coloniale: la caféiculture au Kenya, in TULET, J.-Ch., CHARLERY, B., BART, F. & PILLEBOUE, J. (eds.), *Paysanneries du café des hautes terres tropicales*, Paris, Karthla, p. 68-93.

BATIBO, H., et MARTIN, D., (eds.), 1989, *Tanzanie. L'ujamaa face aux réalités*, Paris, Editions Recherches sur les Civilisations, Mémoire n° 80.

BUIJTENHUIJS, R., 1971, *Le mouvement 'mau-mau'. Une révolte paysanne et anti-coloniale en Afrique Noire*, Paris, Mouton.

COQUERY-VIDROVITCH, C. et MONIOT, H. 1984 (second edition). *L'Afrique Noire de 1800 à nos jours*, Paris, Presses Universitaires de France. (first published 1974).

CROWDER, M., 1968, *West Africa under colonial rule*, London, Hutchinson.

FREMIGACCI, J., 1982, Les colons de la côte-est centrale de Madagascar, de la prospérité à la crise (1924-1939), *Omaly sy Anio*, 15, p. 125-170.

GULLIVER, P. H., 1963, *Social control in an African society. A study of the Arusha : agricultural Masai of Northern Tanganyika*, London, Routledge & Kegan Paul.

HATUNGIMANA, A., 1993, Les cultures coloniales et les paysanneries africaines : projets et bilans. La caféiculture en Urundi, au Congo Belge et au Tanganyika entre les deux guerres mondiales, Université de Paris I, Mémoire de D.E.A. en histoire.

ILIFFE, J., 1979, *A modern history of Tanganyika*, Cambridge, Cambridge University Press.

JAPHET K., et SEATON, E., 1967, *The Meru Land Case*, Nairobi, East African Publishing House.

LUANDA, N.N., 1986, European commercial farming and its impact on the Meru and Arusha peoples of Tanzania, 1920-1955, University of Cambridge (United Kingdom), Ph. D.

MBISE, A. S., 1973, The evangelist: Matayo Leveriya Kaaya, in ILIFFE, J., (ed.), *Modern Tanzanians. A volume of biographies*, Nairobi, East African Publishing House, p. 27-42.

MOORE, S. F., et PURITT., 1977, *The Chagga and Meru of Tanzania*, London, International African Institute, Ethnographic Survey of Africa, 18.

MOORE, S.F., 1986, *Social facts and fabrications. 'Customary' law on Kilimanjaro, 1880-1980*, Cambridge, Cambridge Univeristy Press.

MOSLEY, P., 1983, *The settlers economies. Studies in the economic history of Kenya and Southern Rhodesia, 1900-1963*, Cambridge, Cambridge University Press.

NELSON, A., 1967, *The Freemen of Meru*, Oxford, Oxford University Press.

PURITT, P., 1970, The Meru of Tanzania: a study of their social and political organization, University of Illinois, Ph. D.

PURITT, P., 1977, The Meru of northeastern Tanzania, in MOORE, S. F., et PURITT, P., *The Chagga and Meru of Tanzania*,

London, International African Institute, Ethnographic Survey of Africa, 18, p. 90-140.

SPEAR, T., 1993, Being ‘Maasai’, but not ‘People of Cattle’. Arusha Agricultural Maasai in the Nineteenth Century, in SPEAR, T. et WALLER, R., eds., *Being Maasai. Ethnicity and Identity in East Africa*. London, James Currey, p. 120-136.

SURET-CANALE, J., 1964, *Afrique Noire occidentale et centrale, t. 2, L’ère coloniale, 1900-1945*, Paris, Editions sociales.

TULET, J.-Ch., CHARLERY, B., BART, F., et PILLEBOU, J., (eds.), 1994, *Paysanneries du café des hautes terres tropicales*, Paris, Karthala.

ZWANENBERG, R.M. Van, (with Anne KING), 1975, *An economic history of Kenya and Uganda, 1800-1970*, London, MacMillan, second edition 1977.